

# KUONDOKA KWA HIARI:

## HATARI, FAIDA, NA KIPI KINACHOBADILIKA MWAKA WA 2025

Kuondoka kwa hiari ni **chaguo halali la kisheria** linalowaruhusu wakimbizi wasiosajiliwa **kuondoka Marekani kwa hiari yao**, badala ya kuvurushwa nje na mamlaka ya uhamiaji. Kama unafikiria kuchukua hatua hii, ni muhimu kwanza kuelewa inamaanisha nini, ni hatari zipi zimo na jinsi ya kuomba nafasi hii



### JE, KUONDOKA KWA HIARI NI NINI?

Kuondoka kwa hiari kunamaanisha kuchagua kuondoka Marekani bila kutolewa makataa ya kuondoka na hakimu

**Jinsi tofauti za kuondoka kwa hiari:**



#### 1. Kabla ya uamuzi :

Unaweza kuuliza kuondoka kwa hiari **kabla ya kupata uamuzi wa mwisho** wa kesi yako ya uhamiaji

Ni rahisi kupata idhini.

#### 2. Baada ya uamuzi:

Unaweza kuuliza kuondoka kwa hiari **mwishoni mwa kesi** yako ya uhamiaji. Hii mara nyingi hummanisha hakimu ametoa uamuzi hutaruhusiwa kuendelea kukaa Marekani, na makataa ya kuondolewa (kuvurishwa nje) yametolewa.

Huwa ni **vigumu sana** kupata idhini.

**Kwa jinsi zote mbili, lazima uulize moja kwa moja kwa hakimu wakati wa kusikizwa kesi yako.** Ili kupata idhini ya kuondoka kwa hiari, lazima:

- Ukubali kuwepo Marekani bila hati za uhamiaji,
- na uondoa ombi au ombi lako la msaada wa uhamiaji (kama bado hujatuma)



### KWA NINI INGENIBIDI NIULIZE KUONDOKA KWA HIARI?

Kama ombi litaidhinishwa, kuondoka kwa hiari kutaondoa kutolewa kwa makataa ya kuondolewa kuwepo kwenye rekodi yako, na hii itaweza kuleta urahisi kwako kuomba manufaa ya uhamiaji, kama vile visa, nyakati za mbeleni.

Walakini, kuondoka kwa hiari kunaweza pia kuwa na madhara mabaya kwa kesi yako ya uhamiaji nyakati za mbeleni. Endelea kusoma ili kuelewa baadhi ya hatari.

### JE NI HATARI ZIPI?

1. ama umekuwa Marekani bila stakabadhi kwa zaidi ya mwaka, kuondoka kwa hiari kunaweza **kuchochea marufuku ya kutorudi Marekani kwa muda wa miaka kumi.** Elewa: hii haiwalengi wadogo wa umri. Kama utaondoka Marekani kabla ya kufikisha miaka 18, hutatia kumbukumbu ya uwepo usio halali.



2. Inaweza kukubidi **kuachilia nafasi ya kuomba uhifadhi** au ulinzi mwingine wa kisheria



3. Kwa kesi nyingi, unaweza kuhitajika **kugharamia usafiri wa kurudi** nchi yako ya asili.



4. Kama hutaondoka kwa wakati, unaweza kupigwa **faini ya hadi \$998 kwa kila siku** na upigwe marufuku ya kutorejea tena Marekani.



### ULIGANIFU KUJIHAMI NA KUONDOKA KWA HIARI ?

Tahadhari: Ijapokuwa maneno haya yanasikika kama sawa, **haina usawa wowote:**

**Kujihami** ni usemi **usio rasmi**. Kwa kawaida inamaanisha **unaweza kuondoka Marekani kwa hiari yako, bila ruhusa kutoka kwa hakimu.** Kujihami kunaweza na **hatari** sawa na zile za kuondoka kwa hiari. Na juu ya hatari hizi, kuna uwezekano utakuwa na pendekezo la kuondolewa.

**VS**

Kumbuka, **kuondoka kwa hiari** ni **mchakato rasmi wa kisheria ulioidhinishwa na hakimu wa uhamiaji.** Lazima uhitimisha baadhi ya matakwa na uondoka kwa wakati uliowekwa. Kama utafuata maagizo, utazuia ilani ya kuvuruskwa kwenye kumbukumbu ya rekodi yako.

### JE, NI YAPI MAPYA 2025?

Mnamo Mei 5, Rais Trump alitangaza **utaratibu mpya wa program ya kujiondoa kwa hiari kupitia CBP Home App.** Wahamiaji walio Marekani bila stakabadhi wanaweza kutumia CBP Home App kutuma fomu ya "kusudio la kuondoka"

**Onyo:** Programu hii inadai kupokeza posho ya \$1000, kugharamia hasara za usafiri, na kukatisha kutolewa hatua (kama kutiwa korokoroni) kwa wale wanaohiari kuondoka (kuondoka kwa hiari yao). Walakini, **hamna dhamana ya kisheria** kuwa \$1000 itatolewa au uhamiaji utatendeka kwa hali shwari na ubinadamu

**Muhimu kutambua:** ingawa umesikia manaeno "kuondoka kwa hiari", **program hii ni njia moja ya kujihami.** Programu hii si sawa na ukawaida wa kuondoka kwa hiari ulioidhinishwa na hakimu.

Mchakato huu **sio ya uhalali wa faida za kisheria za uhamiaji** na **haulindi uwezekano wako wa kurudi tena Marekani** siku za mbeleni.

### JE, ITABIDI NIFANYE NINI?



**Zungumza na wakili wa uhamiaji** kabla ya kutoa uamuzi kuhusu kuondoka kwa hiari au kujihami. Wakili anaweza kukusaidia kuelewa haki zako na jinsi kuondoka kwa hiari kunavyoweza kuathiri kesi yako ya uhamiaji.

- **Fahamu:** Usitie Saini yoyote kabla ya kuongea na wakili
- **Elewa haki zako!** Kumbuka, una haki ya kunyamaza kimya, na haki ya kupata mwanasheria.